



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1))

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya BIHARAMULO anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya Shiling **734,922,103.79** (millioni mia saba thelathini na nne laki tisa na ishirini na mbili elfu mia moja na tatu na senti sabini na tisa) zimetengwa katika robo ya pili ya Oktoba-Desemba 2024. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuomba mkopo na kuwasilisha maombi ya mkopo huo katika Ofisi za Serikali za Mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mkopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P. 70, Biharamulo, Simu:0282225003, Nukushi: 0282225216,
Barua pepe: ded@biharamulodc.go.tz, Tovuti: www.biharamulodc.go.tz

- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kijasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.


Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;-

1. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa kijiji/mtaa,
2. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo,
3. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na;
4. Taarifa ya akaunti ya benki (Bank Statement).

NB: Ili kikundi kiweze kusajiliwa kwa ajili ya kupata mkopo ni lazima kiwe na nyaraka zifuatazo:-

- i. Barua ya utambulisho wa kikundi kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa wa eneo husika,
- ii. Katiba ya kikundi ikiambatishwa na wasifu wa viongozi wa kikundi (Mwenyekiti, Katibu na Mhasibu),
- iii. Muhtasari wa kikundi wa kuomba kusajiliwa ukiambatishwa na mahudhurio ya wanakikundi,
- iv. Barua ya kikundi ya kuomba kusajiliwa (barua hii iandikwe na wanakikundi) na,
- v. Wanakikundi wote lazima wawe na namba za NIDA.

Tangazo hili limetolewa na: -


Innocent Mbandwa Mukandala
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BIHARAMULO

MKURUGENZI MTENDAJI
BIHARAMULO
WAZO